

WIMBO WA TAIFA LA TANZANIA

MUNGU IBARIKI AFRICA
WABARIKI VIONGOZI WAKE
HEKIMA PAMOJA NA AMANI
HIZI NI NGAO ZETU
AFRICA NA WATU WAKE

IBARIKI AFRIKA, IBARIKI ARIKA
TUBARIKI WATOTO WA AFRIKA

MUNGU IBARIKI TANZANIA
DUMISHA UHURU NA UMOJA
WAKE NA WAUME NA WATOTO
MUNGU IBARIKI
TANZANIA NA WATU WAKE

IBARIKI AFRIKA, IBARIKI ARIKA
TUBARIKI WATOTO WA AFRIKA

TAARIFA YA BENDERA

Bendera ya taifa letu la TANZANIA lazima ipewe heshima na umuhimu unaostahili. Haifai kupeperusha bendera usiku kwani hakuna anayeweza kuiona pasipo mwangaza Huku kupeperusha bendera usiku hudhoufisha maisha ya bendera maradufu. Wakati bendera inaposhushwa jioni, iwapo kuna mvua tandaza bendera yenyewe chini ili iweze kukauka kabisa kabla ya kuikunja

ITIFAKI YA BENDERA

1. Iwapo bendera ya Taifa inapeperushwa, ni lazima iwe katika mlingoti mwandamizi
2. Mlingoti mwandamizi ni (a) Mlingoti wa juu kabisa uwe katika kundi, (b) Mlingoti ikiwa katika mstari(mjengo ikiwa nyuma yako) mlingoti mwandamizi uko upande wa kulia wa mstari. (Ukizilangalia ni upande wa kushoto)
3. Usipeperusha kamwe bendera moja juu ya nyingine katika mlingoti mmoja, kwani kwa kufanya hivi bendera iliyoko chini itakuwa imetekwa na bendera iliyoko juu yake.
4. Si Kawaida kupeperusha bendera mbili tofauti katika mlingoti mmoja na kwenya kimo au urefu sawa, kwani bendera hazipeperuki vyema wala hazitatambuliki.
5. Bendera ya taifa la TANZANIA huwa kipaumbele, dhidi ya bendera za kampuni ambazo huchukua kipaumbele dhidi, ya bendera za vitengo fulani.
6. Licha ya yaliyojawa katika ibara ya tano kuhusukupa bendera kipaumbele hakuna jambo lolote limeandikishwa na kuthibitishwa. Iwapo bendera nyingi zinapeperushwa Basi watu wengi huipa bendera ya jumuiya ya madola kipaumbele kishaa bendera za Mataifa mengine ya Kigeni na hatimaye bendera hufuatana na mpango wa alfabeti.
7. Haifai kwa vyovyote vile kutumia bendera ya taifa la TANZANIA kibiashara, kuongeza nembu au alama yoyote ile.
8. Daima peperusha bendera safi, na upandishe juu kabisa kwenye mlingoti.
9. Kamwe usipeperusha bendera nusu mlingoti. Ikipokuwa siku ya maombolezo ya kitaifa kwa amri ya serikali.
10. Wakati bendera iliyokuwa nusu mlingoti yateremushwa ni sharti ipandishe juu hadi mwisho wa mlingoti kisha ulteremusha chini.
11. Iwapo haiwezekani kupandisha bendera zote zilizo na vilevile kuziteremusha kwa wakati mmoja, basi ni bora kuipandisha bendera ya taifa mwanzo na kuteremusha ikiwa ya mwisho baada ya zingine zote.
12. Usitumie bendera ya taifa kama kitambaa cha meza kwenye mikutano ya umma. Yafaa iwe juu, nyuma ya jukwaa.
13. Usilache mlingoti bila bendera mchana, kwani ni ishara ya kutowajibika.

Hakikisha kuwa bendera ya taifa yapeperushwa ikiwa wima. Rangi za bendera zafaa kufuatana kuanzia iliyoko kando ya mlingoti ni rangi ya kijani kisha rangi ya njano ikiifuatana nyeusi kisha njano hatimaye biru.

